

**1986:** Allyekuw Rals wa serikali ya Makaburu Afrika Kusini, Pieter W. Botha amtuma waziri wake wa sheria kwenda kumzuru Nelson Mandela kifungoni.



**1975:** Mohamed Ali amtwangwa kwa Knock out Ron Lyle katika raundi ya 11. Ali, raja wa Marekan, anatajwa kama bon-dala mahiril kuwahili kutokea duniani

**11**  
**JUMANNE,**  
**MEI 16, 2023**

MWANANCHI UK 11



HABEL CHIDAWALI.

**H**ivi karibuni Wizara ya Mifugo na Uvvi ilipitishiwa bajeti yake kwa mwaka 2023/24, ambapo kiasi cha Sh295.9 bilioni zimeombwa katika sekta zote mbili.

Ulikuwa ni mnyukano wa hoja baada ya wabunge kuonesha uchungu wao katika kuwatetea wafugaji nchini, na kwa sauti za juu walipaza wakisema wafugaji ni kundi muhimu lakini limesesaulika.

Miongoni mwa mambo yanayolamili-ka na wabunge ni faini ya mifugo inayoingia kwenye hifadhi, kukosekana kwa malisho bora, uvishaji wa hereni kwa wanyama, uuzaji wa mifugo bila kutumia mizani. Pia urejeshaji wa mifugo ambayo wafugaji wanashinda kesi lakini mifugo yao hairudishwi.

Wafugaji wanashi kwa sonona; hawa-na amani katika maeneo yao licha ya kauli za kuwatetea zinazoendelea kutolewa na viongozi wa juu, lakini utekelezaji wake kuu mgumu kwa kada ya chini.

Ongezeko la watu linalochanga ukujai wa miji ni shughuli za binadamu iki-wemo mabadiliko ya tabia nchi, vinatjawa chanzo cha kukosa maeneo ya kuchungia mifugo na majosho ya kuogesha wanyama lakini hata mapito.

Lakini pia utashi wa kisasa unakoseka-na kutoka kwa baadhi ya wenyewe mamlaka, ambao wameamua kuweka pamba masikioni ili kuonesha kuwa hawasikii wala kujali kuhusu kinachoitwa mifugo lakini wanajua kuna umuhimu wa kula nyama.

Hivi karibuni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa agizo lillolenga kumiliza tatio au kupunguza migogoro ambalo alilitupa kwa wakuu wa mikoa na wilaya jijini Dodoma, akiwataa viongozi hao waende kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo na kuwakabidihi wafugaji.

Majaliwa alisema kutenga maeneo ni njia mojawapo itakayosaidia kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji, ambayo ni kuwatengenea maeneo wafugaji ili wadumu katika maeneo yao na kupelekewa miundombini.

Agizo hilo halijatekeleza, limebaki likilea bila usimamizi wa karibu badala yake Watanzania wanaendelea kuwa na mvutano, huku kundi la wafugaji likiwa na macho mengi kuliko kundi la upande wa pili.

Ni linii wafugaji wataishi kwa uhuru katika nchi yao badala ya kuishi kwa kukiimbizwa kila mahali, huku kukiwa na sauti za kutaja namna gani wanasaidiwa lakini hakuna kinachofanana na ukweli wake?

Mfano mwiningine ni katika Mkoa wa Dodoma ambako fursa ilikuja miguuni kwa kiwanda cha mbolea cha Itracom Kilichojengwa eneo la Nala ambacho kitazalisha mbolea zaidi ya tani 60,000.

Hiki ndicho kiwanda kilichotangaza kutumia samadi kutoka kwenye mazizi

## Sio siri nchi hii tunawabagua wafugaji

ya wafugaji katika mkoa wa Dodoma, ambapo wafugaji wanatengeneza fedha huko mifugo ikibaki kwa faida nyingine.

Wafugaji walijua neema imewafuata miguuni lakini wenyewe kiwanda waliamini kupata malighafi kwa karibu. Yote yameota mbawa kwani mifugaji hana nafasi ya karibu kuuza mbolea lakini wenyewe viwanda kufuata samadi mbali.

Moja ya wilaya zilizoathirika zaidi ni Bahi ambayo wafugaji wa vijiji ya Mayamaya na Kongogo wanekutana na kinachoitwa maendeleo, ambayo kwa namna nyinyi yanawatenga moja kwa moja kwani wanatakiwa kupisha bila maelezo waende wapi.

Ardhi walijoutumia wafugaji kwa ajili ya kuchunga mifugo kwenye vijiji hivi iko mikononi mwa watu, baadhi ni wenyewe, madaraka na matajiri walionunua na kuanzisha miradi mikubwa ya kilimo.

Njia zinazotumiwa na wafugaji zime-fungwa, visima vya asili viliviyotumiwa kwa ajili ya mifugo vimejazwa udongo

**Wafugaji wanapaswa kuyakimbia makao makuu kwenda maeneo ambayo hadi sasa hawaajaambili ni wapi.**

na maeneo yake kuanzisha shughuli za kilimo na ujenzi. Wafugaji wanapelekwa wapi?

Ni kwa nini maendeleo yanapokua yanapelekwa faida kwa kundi moja lakini wafugaji hawatajwi kwa uzito wake, au ndio kusema bado tunaamini Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi kwenye ile alama ya jembe na nyundo?

Kilio cha wafugaji si kuambiwa wapishe maeneo, lakini wanajiuiliza ni wapi wanakopelekwa na mifugo yao, hakuna sauti inayotoka kwa kiongozi au mtu wa kawaada isipokuwa mvumo wa kuambiwa waondoke. Je, hawatakiwi nchini?

Serikali itazame jambo hili. Wanayo wizara lakini mifugo ilikamatwa, inase-ma haisiusiki na jambo hilo, inakuwaje maendeleo yabagie watu?

Mko wa Dodoma ni miongoni mwa waathirika wakubwa. Wafugaji wanapaswa kuyakimbia makao makuu kwenda maeneo ambayo hadi sasa hawaajaambili wa ni wapi.

Baada ya ujio wa makao makuu, wakazi wa maeneo hayo ambao kwa sehemu kubwa ni wafugaji na wakulima, hawa-jaambiwa pakwendwa licha. Serikali kusema maeneo yaliyopo si ya kifugaji tena.

Huu ni wakati wa kulfazama kundi hili, haiwezekani kila wakati maendeleo yawayakataa wafugaji. Tuwanusuru kwani nao ni sehemu muhimu ya Taifa.

**Habel Chidawali ni mwandishi wa Mwananchi mkoani Dodoma. hchi-dawali@mwananchi.co.tz**